Jarida la Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

# SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi

Ifanye haki
Iwe shauku

Toleo Na. 004 Jarida la kila miezi mitatu Oktoba - Disemba, 2010

# ZLSC yaendelea kutekeleza Mpango wa Kazi

KITUO cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kimefanikiwa kutekeleza Mpango Kazi *(strategic plan)* wa miaka minne kutoka mwaka 2008 hadi mwaka 2011 kwa asilimia 80.

Mkurugenzi wa Kituo, Bwana Iss-haq Ismail Shariff alisema wanatarajia Mpango Kazi utakamilishwa kwa asilimia 100 ifikapo mwako ujao.

''Tunaamini tutakamilisha asilimia 100 ya Mpango Kazi ifikapo mwaka ujao,'' alisema Mkurugenzi.

Alitaja baadhi ya mafanikio ni kutoa elimu ya wasaidizi wa sheria *(paralegals)* 52 waliopo katika majimbo 50 ya uchaguzi Unguja na Pemba. Alisema wasaidizi wa sheria wanapewa mafunzo ya sheria ya miaka miwili ili kuwawezesha kutoa msaada wa sheria.

Aidha, alisema mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kutoa msaada wa sheria kwa walengwa hususan wasiojiweza, kuajiri maafisa wa mipango *(programme officers)* katika afisi za Kituo ziliopo Unguja na Pemba na kutembelea magereza ili kutathmini utekelezaji wa haki za binadamu.

Kituo kimeweza kutoa mafunzo ya haki za binadamu kwa taasisi mbali mbali za kiraia na Serikali Zanzibar.

Vile vile, Kituo kimeweza kutoa ripoti za haki ya binadamu kwa kila mwaka kuanzia mwaka 2006, kuchapisha Jarida la Kituo *''Sheria na Haki'',* kuendesha vipindi vya elimu ya sheria katika televisheni na redio za umma na binafsi na kuangalia uchaguzi mkuu wa Zanzibar uliofanyika mwaka 2010.

Inaendelea Uk. 3



YALIYOMO

- Tahariri Uk. 2
- Wananchi wenye matatizo ya sheria wasaidiwa Uk. 3
- Mgawanyo wa mali baada ya talaka ni kikwazo kwa wanawake Uk. 4
- MV Mapinduzi Uk. 5
- Uteuzi wa majaji zanzibar waleta malalamiko Uk. 8
- Kosa la kubaka Uk. 10
- Kituo kimeadhamisha Siku ya Kuzaliwa Prof. Haroub Othman Uk. 12
- ZEC yatakiwa kuendesha uchaguzi kwa uwazi Uk. 14
- Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (1999) Uk. 15
- Akatwa sikio na mashoga zake Uk.16

# Zijue sheria zilizopitishwa 2010

**BARAZA la Wawakilishi la Zanzibar limepitisha jumla ya sheria kumi na moja katika mwaka wa 2010 na kusainiwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume.Sheria zilizopitishwa ni hizi zifuatazo:**

(1) *The Zanzibar Broadcasting Commission (Amendment) Act* No 1 ya mwaka 2010. Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar tarehe 20-01-2010.

(2) *The Office of the Director of Public Prosecutions Act No* 2 ya mwaka 2010. Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar tarehe 22-01-2010.

(3) *The Government Proceedings Act No* 3 ya mwaka 2010. Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar tarehe 24-03-2010.

(4) *The Stone Town Conservation and Development Authority Act No* 4 ya

Inaendelea Uk. 3

Ajenda ya watoto Zanzibar:-

1. Wekeza kuokoa maisha ya watoto na wanawake

## Bodi ya Wahariri


**Mhariri:** Prof. Chris Maina Peter

**Msaidizi Mhariri:** Iss-haq I. Shariff

**Mwenyekiti:** Harusi M. Mpatani

**Wajumbe:**
Ali Uki
Safia M. Khamis
**Msanifu**
Yussuf A. Hassan

Ifanye haki



Iwe shauku

*Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa:*
***Simu:*** *0242233784*
***P.O.Box:*** *3360 Zanzibar*
***Fax:*** *0242234495*
***E-mail:*** *zlsc@hudumazasheria.or.tz*
***website:****www.hudumazasheria.or.tz*

Wananchi wote mnaombwa kusoma Jarida hili la Kituo kwa madhumuni ya kujifunza zaidi na kupima maendeleo ya utendaji kazi za Kituo.
Tunakaribisha barua za maoni kutoka kwa wasomaji na michango ya makala kwa ajili ya kuelimisha umma.
Aidha wote watakaopenda kuchangia au kuleta maoni yao katika Jarida la Sheria na Haki wanatakiwa wajitambulishe kwa majina pamoja na anuani zao ili kuleta ufanisi, ukweli na uwezi katika kuendeleza Jarida hili.
Bodi ya Wahariri itakuwa na uwezo wa mwisho wa kuamua au kuhariri habari itakayochapishwa kwenye Jarida hili.Mhariri.

## Tahariri

# Sheria za ardhi ziheshimiwe Zanzibar



TAKWIMU na tafiti mbali zilizofanywa na asasi za kiraia Zanzibar na taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeonyesha kuongezeka kwa wimbi kubwa la migogoro ya ardhi inayowajumuisha wananchi kwa wananchi au taasisi za serikali na wananchi.

Sababu mbali mbali za kuongezeka kwa wimbi la migogoro ya ardhi zimetolewa ikiwemo kasi ya maendeleo ya sekta ya ujenzi ili kujitafutia makazi bora, kuimarika kwa sekta ya kilimo na ongezeko la uwekezaji wa vitega uchumi hususan katika sekta ya utalii ambayo imepamba moto.

Kwanza kabisa tungependa kuweka wazi msimamo wetu kwamba tunaunga mkono hatua za maendeleo zinayofanywa na Serikali au wananchi ili kuitoa nchi na wananchi katika dimbwi la umaskini. Vile vile, tunaamini kwamba ardhi ni rasilimali muhimu inayoongezeka thamani kila siku na ili tuendelee basi tunahitaji ardhi pamoja na siasa safi, uongozi bora na watu.

Lakini jambo linalotukera ni kwamba kasi ya maendeleo kupitia rasilimali ardhi haiendi sambamba na mipango bora ya maendeleo. Badala yake kumejichomoza migogoro ya ardhi katika sehemu zote za visiwa vya Unguja na Pemba husussan katika fukwe za bahari ya Hindi iliyoizunguka Zanzibar.

Migogoro ya ardhi tunayoikusudia hapa sio ile ya mtu mmoja anayejenga nyumba ya kuishi kuamua kuongeza mita chache katika eneo la jirani yake. La hasha. Migogoro tunayoisema hapa ni kuona pande kubwa la ardhi lililokuwa chini ya usimamizi wa mwananchi au wananchi wa kijiji fulani kuchukuliwa na kupewa mtu mwengine kwa visingizio tofauti.

Vilio vya wananchi kuhusu ardhi vimesambaa kila pembe. Baadhi ya wananchi wanalalamika kwamba ardhi ama waliyorithi kutoka kwa wazee wao au waliyopewa na Serikali baada ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964, wananyang'anywa tena kinyume na taratibu za Sheria za Ardhi zilizotungwa kupitia Baraza la Wawakilishi na wala sio chini ya utawala wa kikoloni.

Jambo la kusikitisha ni kwamba wanaoshutumiwa kuwa mstari wa mbele wa migogoro ya ardhi ni baadhi ya viongozi wa taasisi za serikali kwa kutumia vibaya madaraka waliyopewa hutoa amri zisizo halali ya ardhi kuhamishwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwengine, kufuta hati bila ya kufuata taratibu na kuwamilikisha watu wengine. Wakati mwingine hao hao wenye mamlaka au rafiki na ndugu zao wanaoamua kubinafsisha na kujenga sehemu za wazi na viwanja vya kuchezea watoto kwa makusudi kabisa.

Tunafahamu fika kwamba ardhi yote ni mali ya umma na ipo chini ya usimamizi wa Serikali na Wazanzibari wanapewa haki ya matumizi ya ardhi tu. Lakini sheria hizo hizo za ardhi zimeeleza utaratibu madhubuti wa kuhamisha ardhi kwa maslahi ya umma ikiwemo kupatikana ridhaa ya Mahkama ya Ardhi, jambo ambalo haliheshimiwi.

Ijapokuwa tafsiri ya msamiati maslahi ya umma kisheria ni pana lakini inaonekana wajanja wachache hutumia mwanya huu pamoja na madaraka waliyopewa kuwadhulumu ardhi wengine na hasa wanyonge kwa njia zisizo halali ikiwemo vitisho.

Tunawahimiza wale wote wanaohisi haki zao za kumiliki ardhi zimekiukwa wapeleke malalamiko katika Mahkama ya Ardhi. Lakini tunaiomba Serikali kupitia wawakilishi wake katika taasisi mbali mbali kutimiza wajibu wao kwa kufuata sheria na kuacha kutumia madaraka yao vibaya na kwa maslahi yao binafsi.

Vile vile, tunaiomba Serikali kuongeza wahusika wa usuluhishi wa migogoro ya ardhi ikiwezekana katika kila Wilaya ili kupunguza mzigo mkubwa wa kesi za ardhi zilizorundikana ambazo aidha zinakwenda kwa mwendo wa konokono au zinapigwa kalenda kila kukicha.

**Prof. Chris Maina Peter**
**Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini**
**Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar**

# Wananchi wenye matatizo ya sheria wasaidiwa



IDADI ndogo ya wananchi wenye matatizo ya sheria wamejitokeza kupata msaada wa kisheria ambao ulitolewa bure Disemba 13, 2010 katika kijiji cha Kiboje, Shehia ya Mkwajuni, Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja.

Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kwa kushirikana na Jumuiya nyengine za wanasheria Zanzibar hutoa msaada wa bure wa sheria kwa wananchi wa Zanzibar kila Disemba 13 ya kila mwaka ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha siku ya Msaada wa Sheria duniani.

Jumla ya watu 18 walijitokeza kupata msaada wa sheria katika kijiji hicho. Kesi zilizoripotiwa ni migogoro ya ardhi, familia, utoroshwaji wa watoto na matunzo ya watoto.

Afisa Mipango wa ZLSC, Bwana Rashid Abdallah alisema inaonekana kwamba mwamko wa kufahamu sheria bado ni mdogo na watu wengi hupendelea kumaliza kesi kienyeji hususan kesi za ubakaji ambazo zimekuwa zikiongezeka kwa kasi.

Aliwashauri wananchi kujitokeza kwa wingi kupata msaada wa sheria hususan wale wasiokuwa na uwezo wa kuajiri wakili kusimamia kesi zao.

''Milango ya Kituo chetu ipo wazi. Njooni mpate msaada wa bure wa sheria ili mtatue matatizo yenu kisheria badala ya kumaliza kwa njia za kienyeji,'' alisema Bwana Rashid.

Alisema Kituo kimeanzishwa mwaka 1992 kwa madhumuni ya kutoa msaada wa sheria kwa wasiojiweza ili wasidhulumiwe na kuonewa.

Sheha wa Shehia ya Kiboje Mkwajuni Bwana Mabrouk Juma Khamis alisema matatizo ya sheria yanawakabili wanavijiji lakini inaonekana watu wana hofu ya kujitokeza kupata msaada wa sheria.

''Tunamaliza matatizo kienyeji kwasababu tunaoneana vibaya,'' alisema Sheha huyo.

Alikiomba Kituo kupanga taratibu za kuwatembelea mara kwa mara ili kutoa msaada wa sheria kwa wananchi.

Vile vile msaada wa kisheria ulitolewa katika kijiji cha Tumbe, Mkowa wa Kaskazini Pemba.

# ZLSC yatimiza malengo

*Inatoka Uk. 1*

Hata hivyo, alisema Kituo kilikabiliwa na matatizo kadhaa yaliyopunguza kasi ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa mwaka 2010.

Aliyataja baadhi ya matatizo hayo ni tatizo la ukosefu wa umeme ulioikumba Zanzibar kwa kipindi cha miezi mitatu na wasaidizi wa sheria pamoja na maafisa wa mipango kushiriki katika zoezi la utazamaji wa uchaguzi.

# Baraza la Wawakilishi

*Inatoka Uk. 1*

**mwaka 2010. Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar tarehe 25-03-2010.**

**(5) *The Zanzibar Sports Council Act No* 5 ya mwaka 2010. Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar tarehe 26-03-2010 na kuanza kutumika tarehe 26-07-2010.**

**(6) *The Referendum Act No* 6. Ya mwaka 2010. Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar tarehe 30-03-2010.**

**(7) *The Fisheries Act No* 7 ya 2010. Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar tarehe 31-03-2010.**

**(8) *The Appropriation Act No* 8 ya mwaka 2010. Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar tarehe 24-6-2010.**

**(9) Sheria ya Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar No 9. Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar tarehe 09-08-2010.**

**(10) Sheria ya Marekebisho ya Umiliki Ardhi, Nam. 12 – Nam 10 ya mwaka 1992. Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 07-08-2010.**

**(11) Sheria ya Kondominio ya Zanzibar Nam 11 ya mwaka 2010 na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi tareheh 07-08-2010.**

# Mgawanyo wa mali baada ya talaka ni kikwazo kwa wanawake

Na Mtumwa Sandal

**UTANGULIZI**

**NDOA** na mahusiano ya kifamilia ni mambo yanayogusa hisia za watu wengi katika jamii. Athari ya mahusiano haya ni kwa wahusika wa ndoa na wanafamilia kwa jumla. Kwa mfano, talaka, kutengana, matunzo ya watoto na pia mgawanyo wa mali zilizochumwa na wanandoa katika wakati wa ndoa.

Suala kubwa linaloumiza vichwa vya wanajamii ni mgawanyo wa mali iliyochumwa na wahusika wakati wa ndoa. Jambo hili mbali na ukubwa wake lakini pia limekuwa likiwatesa na kuwaliza wanawake wengi katika jamii zetu pindi wanapoachika Tatizo la kukosa haki ya kumiliki mali za ndoa kwa wanawake walioachika linawaliza sana kwasababu husaidia kipato na kuchangia kwa nia ya kujenga familia bila ya kujali umiliki madhubuti pindi ndoa itakapovunjika.

Mara nyingi wanawake kwa moyo wao wa huruma, mapenzi na kwa lengo la kuimarisha ndoa zao wamekuwa wakichangia kwa ukamilifu wa hali na mali katika shughuli za kuendeleza maisha na familia. Lakini pindi wanapoachika huwa ni mwisho wa nguvu na jasho lake alilolitumia katika kuimarisha familia na mchango wake hauonekani wa thamani tena.


Mwanamke huachika katika ndoa na kunyimwa haki ya kumiliki mali waliyoichuma yeye na aliyekuwa mume wake. Badala yake wanawake wengi wanashuhudia mali hizo zikitumiwa na kustawishwa na wanawake wengine ambao wameolewa baada yake. Jambo hili linawatia tafrani wanawake na kuwasababishia ugumu wa maisha. Linaloumiza zaidi ni kukosa msaada wa kisheria.

Mwanamke anapokosa haki yake ya kumiliki mali alizochuma na mume wake humuingiza katika dimbwi la umasikini na kukosa njia bora za kuwalea watoto. Mazingira ya aina hii husababisha asilimia kubwa ya wanawake kujiingiza katika vitendo vya ukahaba ili wapate fedha za kumudu gharama za maisha.

**NINI MAANA YA MALI ZILIZOCHUMWA NDANI YA NDOA?**

Katika kesi ya *Watchtel v Wachtel* (1973) FAM 72,90 Lord Denning ameeleza maana ya mali zilizochumwa ndani ya ndoa ni mali ambazo zimechumwa au kupatikana kwa juhudi za mmoja wa wanandoa au kwa juhudi za pamoja kwa lengo la kutumia katika maisha yao ya ndoa.

Hivyo ikitokea wanandoa hawa wameachana mali hizo ni lazima zigawiwe na Mahkama kulingana na kiasi ambacho wanandoa hao wamechangia katika juhudi za kupatikana, kuzilinda na hata kuziendeleza. Mfano wa mali hizo ni nyumba, kiwanja, mashamba, gari, samani za ndani na mifugo.



*Baadhi ya wanawake hudhulumiwa mali baada ya kuachwa*

**SHERIA YA KUGAWA MALI BAADA YA TALAKA**

Kwa Tanzania Bara Sheria inayohusika na masula ya ndoa na ugawaji wa mali za ndoa baada ya talaka ni Kifungu cha 114 (2) cha Sheria ya Ndoa Namb. 5 ya mwaka 1971 kimeeleza wazi juu ya ugawaji wa mali zilizochumwa ndani ya ndoa kuwa zitagawiwa na Mahkama baada ya kutoa talaka kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

a) Mila za jamii ya mke au mume
b) Kiasi cha fedha, mali au kazi kilichochangiwa na kila mwanandoa katika kupatikana mali hizo.
c) Madeni aliyonayo kila mmoja wao ambayo yalipatikana kwa maslahi ya wote.
d) Mahitaji ya watoto wadogo wa ndoa kama wapo.

**NI MALI ZIPI MAHKAMA INASTAHIKI KUZIGAWA KWA WANANDOA?**

Kisheria mali ambazo Mahkama itazigawa kwa wanandoa baada ya kutolewa kwa talaka ni za aina mbili. Aina ya kwanza ni mali zilizopatikana kwa juhudi za pamoja za wanandoa na aina ya pili ni mali inayomilikiwa na mmoja wa wanandoa lakini iliimarishwa na mwanandoa mwezake wakati wa ndoa.

**MALI ILIYOPATIKANA KWA JUHUDI YA PAMOJA.**

Hizi ni aina ya mali zote zilizonunuliwa au kupatikana baada ya wanandoa hao kuingia katika ndoa. Vile vile, wanandoa wote kwa pamoja wawe wamechangia katika kuzilinda na kuzitunza mali hizo. Kwa mazingira haya, Sheria hii ya ndoa, ikiwa wanandoa hao wameachana mali hizo lazima zigawiwe sawa kwa wanandoa hao.

**TAFSIRI YA MALI ZILIZOPATIKANA KWA JUHUDI ZA PAMOJA.**

Kifungu cha 114 cha Sheria hii hakijafafanua kwa uwazi juu ya dhana hii na imesababisha utata mkubwa. Majaji wa Mahkama za juu wanaumiza vichwa vyao juu ya tafsiri ya mali zilizopatikana kwa juhudi za pamoja. Kwa ujumla utata huo hujitokeza pale ambapo mwanandoa mmoja hakuchangia kifedha katika kununua mali zilizopatikana ndani ya ndoa. Majaji wa Mahkama za juu wamegawika makundi mawili. Kundi la kwanza ni lisilopenda mabadiliko *(conservative)* na kundi la pili ni linalopenda mabadiliko na maendeleo *(progressive)*

**KUNDI LISILOPENDA MABADILIKO**

Ni kundi ambalo lina mtazamo finyu juu ya maana ya mali zilizopatikana kwa juhudi za pamoja kwa wanandoa. Mawazo ya watu wa kundi hili huamini kwamba mama wa nyumbani ili aweze kuhesabiwa amechangia kuzalisha na kuichuma mali ya ndoa ni lazima awe ametoa mchango wa

Inaendelea Uk. 5



4. Wekeza katika kumkinga mtoto dhidi ya Ukatili, Unyanyasaji na Unyonyaji

# Mgawanyo wa mali baada ya talaka ni kikwazo kwa wanawake

**Inatoka Uk. 4**

kifedha au nguvu zake kama amefanya biashara hata ya kuuza maandazi, chapati, amecheza upatu n.k katika kupatikana kwa mali hizo. Mahkama zimetoa uamuzi wa aina hiyo katika kesi mbali mbali ikiwemo ya *Zawadi Abdallah v Ibrahim Iddi* (1980), TLR 10. Katika kesi hii iliamuliwa kwamba; kwa mama wa nyumbani anayefanya kazi za ndani kama kumpikia mume na watoto chakula, kutunza familia na watoto huwa hana mchango wowote katika kupatikana mali za ndoa na hivyo baada ya kuachana na mumewe hastahiki kupata chochote katika mali zilizopatikana katika ndoa ambazo zimechumwa kwa juhudi za mume wake.

**KUNDI LINALOPENDA MABADILIKO**

Kundi hili linapenda mabadiliko na maendeleo. Majaji wa kundi hili huamini mali zilizopatikana kwa juhudi za pamoja kwa wanandoa hujumuisha hata mchango anaoutoa mama wa nyumbani kama kutunza watoto, mume na familia. Hata kama hajajishughulisha na kazi yoyote au hakuchangia kifedha kupatikana mali za ndoa, anapoachika hana haja ya kuonesha mchango wa moja kwa moja katika kupatikana mali za ndoa. Inatosha kuonesha kuwa alikuwepo nyumbani, akitunza watoto na kufanya kazi nyengine ambazo zinafanywa na akina mama hapo nyumbani.

Moja ya kesi zilizoamuliwa kwa kutumia mawazo haya ni kesi maarufu ya *Bi.Hawa Mohamed v.Ally Sefu* (1983) TLR 32. Iliamuliwa katika kesi kwamba juhudi anazozitoa mama wa nyumbani kama kumtunza mume, watoto na kufanya kazi zote kama anazofanya mama wa nyumbani ni juhudi na mchango wa mama huyo katika kupatikana mali za ndoa. Anapoachika mwanamke wa aina hii anastahiki kupata mali zilizopatikana katika ndoa yake.

Mtazamo huu huegemea na sababu kuwa familia ni kiungo kikubwa sana hivyo mtu ambaye anatunza familia lazima atambulike na kupewa nafasi yake. Pia mume hawezi kufanya kazi kwa ufanisi ikiwa hatakuwa na mtu wa kumtunzia familia yake vizuri. Aidha, ufanisi wa mume unaweza ukaletwa kwa mawazo pamoja na umakini wa mke wake.

**MALI YA MWANANDOA MMOJA ILIYOIMARISHWA NDANI YA NDOA.**

Kifungu cha 56 cha Sheria ya Ndoa No.5 ya 1971 kinafafanua kwamba ndoa si sababu ya kuwafanya wanandoa wasimiliki mali waliyonayo kabla ya ndoa. Mume au mke ana haki ya kumiliki mali kwa jina lake kwa mali ambayo ametoka nayo na ameimiliki kabla ya ndoa. Mali aina hii itabakia kuwa ya mwanandoa huyo na haitabadilika kuwa ya mmoja wa mwanandoa au ya pamoja. Lakini Sheria ya ndoa imeweka mazingira kuwa endapo kutatokea talaka Mahkama ina uwezo wa kuigawa mali ya aina hiyo endapo tu ikithibitika kuwa mali hiyo kwa namna moja au nyengine mmoja wa mwanandoa aliimarisha mali hiyo ndani ya ndoa. Kwa msingi huu mali hiyo itagawiwa kwa kiasi kile kilichoongezeka katika mali ile.

**CHANGAMOTO ZINAZOWAPATA WANAWAKE KATIKA KUMILIKI MALI ZA NDOA BAADA YA TALAKA.**

Changamoto zifuatazo ni vikwazo kwa wanawake wengi katika kupigania haki aina hii-

1. Kukosekana kwa utamaduni wa kuripoti matatizo katika sehemu husika.
2. Ukosefu wa elimu ya sheria kwa wanawake ya kutetea haki zao.
3. Aina ya talaka wanawake wanazopewa na waume zao ni kikwazo. Wanawake Tanzania hupewa talaka sio kwa maandishi bali ni kwa mdomo tu. Aidha talaka nyingi hutoka kutokana na ukatili wa kindoa dhidi ya wanawake. Mwanamke anapata woga wa kwenda Mahkamani kudai haki ya ugawaji wa mali baada ya ndoa kuvunjika. Hatimae huona talaka ni salama yake zaidi. Baadhi ya wanawake hufungua kesi Mahkama Kuu ya Zanzibar kuhusu mgao wa mali lakini baada ya siku chache hufuta kesi kwa hiari zao au kutokwenda Mahkamani kusikiliza maombi yao kutokana na vitisho kutoka kwa waliokuwa waume zao. Mfano wa kesi hizo ni *Jullieta Albatto Moda v. Lazaro Abisai Mangasini* (2005)2, HCZ *(unreported)*. Kesi ilifutwa na Mahkama baada ya mwanammke kufungua maombi Mahkamani na hakuhudhuria tena. Pia kesi ya *Nina Meredith Springle v Abdulla Salim Ali* (2006) 2 HCZ *(unreported)* katika kesi hii mwanamke alifungua ombi la kugawa mali baada ya kuachika lakini kwa sababu anazozijua yeye mwenywe aliiomba Mahakama ifute ombi lake.



4. Utekelezaji wa Sheria ya Ndoa Zanzibar bado ni changamoto. Sheria ya Ndoa Namb. 5 ya mwaka 1971 inayotumika Tanzania Bara bado ni kikwazo Zanzibar. Hakuna sheria maalum ya ugawaji wa mali baada ya mwanamke kuachika Zanzibar. Sheria ya Kiislamu hutumika ambayo inamtaka mume anapomuacha mke ampe zawadi tu na sio mgao wa mali. Mahkama Kuu Zanzibar kwa wasiokuwa waislamu hutumia uzoefu na maamuzi ya kesi mbali mbali zilizohukumiwa na Mahkama ya Rufaani ya Tanzania katika kutoa maamuzi. Hivyo, kutokuwepo kwa sheria ya aina hii Zanzibar huwa ni kikwazo kwa wanawake kupata haki zao na hata wanawake wakienda kudai haki zao katika Mahkama za kawaida, hufunguliwa kesi zao kama kesi za madai ya kawaida.
5. Kukosekana na ushahidi wa maandishi *(documentary evidence)* bado ni kikwazo kwa wanawake kuthibitisha mali kama ni ya mume au mke. Kwa mfano, gari au nyumba ni mali ya mwanamke lakini kwa mapenzi na kuzidiwa akili na mume mali hiyo huandikwa majina ya waume zao. Hivyo, wakati wa kuachana, mwanamke anapojaribu kumdai mumewe mali zake huwa ni kikwazo kwasababu hati zote za umiliki zimeshaandikwa kwa majina ya mume peke yake. Wanawake watafute hati miliki mapema kwa mali zao.
6. Mifumo ya Mahkama iliyokuwepo Zanzibar ni kikwazo kwa wanawake. Masuala yanayohusu haki za ndoa yapo chini ya Mahkama ya Kadhi ya Zanzibar ambayo inatambulika kikatiba na inaundwa chini ya Sheria Nambari 3 ya 1985 sheria za Zanzibar . Lakini kisheria, Mahkama ya Kadhi haina uwezo wa kugawa mali baada ya kuachana kwa wanandoa.
7. Kuwepo kwa mitazamo miwili tofauti juu ya ugawaji wa mali kwa wanandoa pindi wanapoachana. Kwa mfano, tujaalie wanawake wanaofungua kesi ya maombi ya ugawaji wa mali baada ya ndoa wakikutana na majaji wenye mtazamo wa kundi lisilopenda maendeleo ni vigumu mwanamke kupata haki.
8. Umasikini. Kufungua kesi ya kudai haki hadi kukamilika na kutolewa hukumu kunahitaji fedha. Baadhi ya wanawake hawana uwezo hivyo ni kikwazo.

**HITIMISHO**

Ugawaji wa mali baada ya kuvunjika kwa ndoa ni suala linalowaliza na kuwaathiri wanawake walio wengi. Ni bora Serikali zikaweka sheria na hatua madhubuti juu ya suala hili. Jamii kupitia taasisi zinazohusika na masula ya wanawake ziongeze jitihada katika kuwaelimisha wanawake kuweza kuzifahamu haki zao na kuzidai.

# Uhaulishwaji wa mali za Serik

**HIVI** karibuni vyombo mbali mbali vya habari vimeripoti juu ya kuhaulishwa kwa mali mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwemo jengo la Mambo Msiige, Wakfu na Mali ya Amana, Mahkama ya Kazi, Starehe Club , eneo la wazi hapo Forodhani na meli ya MV Mapiduzi.

Kuhaulishwa au kuuzwa kwa mali za Serikali ni jambo la kawaida ambalo hufanyika kila siku pale inapooonekana kua mali hizo zimechakaa na hazina tena tija kwa Serikali. Lakini utekelezaji wake hufanyika kwa kuheshimu utaratibu maalum uliowekwa kwa mujibu wa Sheria za nchi.

Hatuna hakika juu ya utaratibu uliofuatwa katika kuhaulishwa mali hizi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizotajwa hapa. Lakini kimsingi tunahisi na tunatahadharisha kuwa ni jambo la umuhimu mkubwa sana kuangalia kama katika zoezi hili kuanzia mwanzo hadi mwisho kama masuala ya msingi yanayohusiana na Utawala Bora hasa katika suala la Manunuzi na Mauzaji ya Mali za Umma yalizingatiwa na kufuatwa au la.

Suala la Mauzaji au Manunuzi ya Mali za Umma ni moja kati ya mambo ya msingi yanayoangaliwa na ni kigezo muhimu cha kupima kuwepo kwa Utawala Bora au la katika nchi yoyote ile kwani hapa mara nyingi taratibu na sheria hukiukwa aidha kwa makusudi kwa ajili ya maslahi binafsi ya wahusika au kwa kutokujua kutokana na kukosekana sifa na uwezo wa watendaji wa Serikali ambapo hupelekea hasara kubwa kwa Serikali.

Mara nyingi, matatizo mengi yanayojitokeza katika nchi nyingi za Afrika kama vile vita visivyokwisha, umasikini, njaa, maradhi, ukiukwaji wa haki za binadamu nk. huwa yanahusishwa na kukosekana kwa Utawala Bora ambapo aliyewahi kua Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Bwana Koffi Annan aliuelezea“Utawala bora ni moja kati ya vitu muhimu sana katika kuondoa umaskini na kuchochea maendeleo.”

“*Good governance is perhaps the single most important factor in eradicating poverty and promoting development*.”

**Kwa hivyo,utawala bora ni:**

1. Chachu ya maendeleo, amani,utulivu na umoja na utulivu wa kisiasa.

Kwa mantiki hii tunaweza kusema kuwa Utawala Bora kwa ufupi ni:

***“Namna ya kuendesha Utawala katika misingi inayojali demokrasia na uwazi na pia kuwa na uelekeo wa maendeleo ambayo yanaongozwa na wananchi wenyewe kwa uwezeshwaji wa Serikali”.***

Hata hivyo wataalamu wengi wanakubaliana kuwa njia nzuri zaidi ya kuelewa Utawala Bora ni kujua ama kueleza maana ya Utawala mbaya.

Utawala mbaya unatafsiriwa kwa ufupi tu kuwa :

***“Ni pale misingi ya Katiba na Sheria za nchi zinapokiukwa kutozingatiwa, kutotekelezwa ama kupindwa kwa maslahi fulani, maadili ya viongozi na ya jamii yanapokiukwa, panapokuwa hapana uwajibikaji wala uwazi katika kutekeleza shughuli za umma, uongozi unaposhindwa kujali matatizo na matarajio ya wananchi panapokosekana muundo mzuri na mfumo unaoeleweka wa vyombo vya umma na utekelezaji wa shughuli zake, inapokuwa viongozi ni wabadhirifu, wala rushwa, wakwepaji majukumu yao, wanaokosa uaminifu na wanaotumia madaraka yao kwa maslahi yao na sio kwa ajili ya umma”.***

Utawala Bora una misingi mikuu mitatu (3) ambayo ni:-

**i.Demokrasia na Haki za Binadamu.**

Tunapozungumzia suala la Demokrasia hapa kwetu watu wengi huhusisha na masuala ya uchaguzi tu. Hii ni sahihi ila ni mtazamo mwembamba sana wa maana ya neno Demokrasia. Neno hili lina maana pana zaidi ya uchaguzi. Maana ya demokrasia ni kuwashirikisha watu katika maamuzi mbalimbali juu ya mambo yanayowahusu. Hapa kuna demokrasia ya moja kwa moja kama ile ya kutoa maoni kwa njia ya kura ambapo watu huulizwa kama wanaridhia jambo fulani linalotaka kufanywa na Serikali na kama wanaridhia au la hutoa maoni yao; na ile ya pili ni ya uwakilishi ambapo kupitia kwa wawakilishi wao waliowachagua hutoa maoni yao juu ya kukubali au kukataa jambo fulani.

**ii. Mgawanyo wa Madaraka**

Katika nchi au taasisi ni lazima kuwe na mgawanyo wa madaraka. Iwapo madaraka yote yatawekwa kwa mtu mmoja, kuna hatari ya mtu huyo kujiamulia mambo anavyotaka yeye na hapa ndipo tunapoona tawala za kidikteta zinapoanza. Mtu mmoja anapanga au kutunga sheria, anaamua, na anatekeleza mwenyewe yale aliyoyaamua na kuyapanga.

Hii ni hatari na inaweza kusababisha kutokea kwa mambo ambayo hayakubaliki. Mfano mtu anaweza akaamua kutamka kuwa mali fulani haifai kuendelea kubakia kuwa ya Serikali na kutoa amri iuzwe na akaamua kujinunulia yeye mwenyewe. Ni lazima kuwe na mgawanyo wa madaraka mmoja awe na kazi ya kusema mali hii haifai kubakia kuendelea kumilikiwa na Serikali na mwengine atoe amri kua iuzwe na mwengine afanye kazi ya kuuza. Kila mmoja kati ya watu hawa anatakiwa kufanya kazi yake bila ya kuingiliwa kwa namna yoyote ile na chombo au taasisi nyengine.

**iii. Utawala wa Sheria.**

Katika kuendesha zoezi zima hili ni lazima kila kitu kifanywe kwa mujibu wa sheria za nchi na kila mmoja aone kuwa kweli sheria hazikupindwa. Jee, kwa mfano Sheria zetu hapa Zanzibar zinazohusiana na mauzaji ya mali chakavu za Serikali zinasemaje juu ya suala la kuuza mali za aina hiyo. Na jee, zimefuatwa na kutekelezwa kama inavyotakiwa?

Hii inamaanisha kuwa Serikali inapotaka

# kali Zanzibar na Utawala bora

kufanya jambo lolote lile ni lazima izingatie misingi hiyo iliyotajwa hapo juu na mambo yote hayo yafanyike katika misingi ya uwazi *(transparency)* bila ya kificho. Na yule anayetaka kujua zaidi juu ya mchakato mzima ulivyokwenda basi ni haki yake apate habari zote kama zilivyokwenda kuanzia mwanzo hadi mwisho. Hii kwa kiasi kikubwa huondoa ile mianya ya rushwa na ufisadi na pia huondoa manung'uniko yasio ya msingi. Uwazi huondoa malalamiko ,kutoaminiana,fitna na majungu.Aidha hutoa fursa ya ushirikishwaji umma, kukosoana na kukosolewa.

*"Tunapozungumzia misingi ya Uwazi hapa hatuna maana ya kutoa hata zile siri za Serikali hadharani. Katika kuendesha mambo ya umma, uwazi una maana ya kuweka mazingira ambayo kila mtu anaelewa shughuli mbalimbali zinazotendwa na Serikali yao kwa upatikanaji wa taarifa sahihi za kijamii na kiuchumi. Hizi ni muhimu kwa sababu zinatumika katika kutoa maamuzi."*

**Uwazi una vigezo vifuatavyo**

- Kuwepo na kuweza kupatikana taarifa sahihi kuhusu shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii (Access to information). Taarifa hizo ni muhimu kwa vile uchumi wa ulimwengu wa sasa unategemea zaidi taarifa sahihi katika kufanya maamuzi. Nchi ambazo hazina uwazi katika uendeshaji huwezi kupata taarifa za mapato na matumizi ya Serikali na hata za wagonjwa wa baadhi ya maradhi.

Ni lazima tujiulize hapa mambo ya msingi, je kabla ya kuchukuwa hatua iliyofanywa wananchi walishirikishwa kwa namna yoyote ile kutoa maoni yao au katika maamuzi hayo kwa namna yoyote ile?

Jee, vyombo vilivyochukua hatua hiyo vilikuwa na mamlaka kisheria kufanya hivyo? na je, yote hayo yamefanywa kwa mujibu wa Sheria za nchi na katika misingi ya uwazi?

Katika zoezi la uhaulishwaji wa mali hizo tulizozitaja hapo juu tunaamini kuwa zoezi zima lilikua likiongozwa na sheria zifuatazo:-

- *The Public Procurement and Disposal of Public Assets Act No* 9/2005.
- *The Land Transfer (Amendment) Act No* 10/2007.

Chini ya Sheria hizi mbili, suala la kuwepo uwazi wa hali ya juu katika mauzaji au manunuzi yanayofanywa na vyombo vyote vya umma ni jambo ambalo linasisitizwa sana. Pia sheria imeweka bayana ni taasisi ipi inayoweza kufanya uhaulishaji wa mali za Serikali na katika misingi ipi.

Hiki ni kigezo muhimu sana kinachoangaliwa kuweza kujua kama kulikuwa na vimelea vya Utawala Bora katika zoezi zima la mauzaji na, au manunuzi ya mali za umma.

Katika hili inasisitizwa wazi kwamba ni lazima kuwe na zabuni za wazi *(open tender)* ambapo kila mtu anapata nafasi ya wazi ya kushiriki katika zoezi hilo.

Hata hivyo hatuelezwi kama katika zoezi hili la uhaulishwaji wa mali hizo zilizotajwa kama sheria na utaratibu unaohitajika uliheshimiwa. Mazingira ya uhaulishwaji wa mali hizi hayakuekwa wazi kiasi cha wananchi wa kawaida na hata taasisi zisizo za kiserikali kuweza kutoa michango yao katika zoezi hili. Inaonekana kuwa zoezi zima hili limegubikwa na usiri mkubwa sana kiasi ambacho ni vigumu kufahamu utaratibu uliotumika kuwapata wazabuni.

Hili linasababisha kuwepo kwa manun'guniko mengi sana kutoka kwa wananchi, taasisi mbalimbali za ndani na nje jinsi zoezi zima lilivyoendeshwa jambo ambalo lingeliweza kuepukwa kama kungelikuwa na uwazi katika mchakato mzima wa utoaji wa mali hizo.


Wananchi wana haki ya msingi ya kuhoji na kupewa taarifa sahihi juu ya mambo mbali mbali yanayofanyika nchini mwao. Hii haina maana ya kwamba wananchi wapewe hata zile taarifa za siri za Serikali. La hasha. Ila zile taarifa za mambo muhimu yanayofanyika kama kitendo cha kuuzwa kwa mali zao (za umma) kama vile:-

- Ni nani aliyepata zabuni? na katika utaratibu upi? Na kwa misingi ipi?
- Bei ambayo mali imeuzwa/ kukodishwa na utaratibu wa malipo?
- Lini kikao/vikao vya zabuni vilifanyika? na washiriki gani? na kumbukumbu zipo wapi?

Tunatarajia taasisi husika zitatoa taarifa kamili ya kuhaulishwa kwa mali hizi kwa umma ili wananchi waweze kuja kama zimetolewa katika misingi inayokubalika na kwa maslahi ya Taifa.

Na ikiwa hakuna taarifa za kutosheleza misingi ya Utawala Bora ni vyema ikafuatwa ili mambo kama haya yasije yakatokea tena kama ambavyo yanatokea kila kukicha kwa majirani zetu kutokana na Serikali kushindwa kufuata misingi ya Utawala bora.

# UTEUZI WA MAJAJI ZANZIBAR WALETA MALALAMIKO



*''Kuna kazi katika jamii zinaweza kufanywa na watu wasiokuwa na nidhamu na heshima zao zinatiliwa mashaka, lakini jaji au hakimu sio miongoni mwa hao.'' NYERERE, Julius K, Hotuba aliyoitoa katika mkutano wa Majaji na Mahakimu uliofanyika Arusha, tarehe 15 Machi, 1984.*

**''There are jobs in our society which can be done by undisciplined people and people whose personal integrity can be called into question, being a judge or magistrate is not among them.'' Nyerere, Julius K, Speech to the meeting of Judges and Magistrates held in Arusha, on 15th March, 1984**

Majaji ni watu muhimu katika nchi wanaopewa uwezo wa Kisheria na Katiba kutekeleza majukumu yao bila ya woga wala upendeleo. Kigezo cha maamuzi ya majaji ni Katiba, sheria na ushahidi unaowasilishwa na pande husika za kesi. Katika utekelezaji wa kazi zao, Majaji wanalazimika kuhakikisha haki inatendeka hata mbingu ikiwa itaanguka (*do justice even if the heaven falls*). Majaji wanaamini kwamba anayestahiki kupewa haki atapewa na asiyestahiki hatopendelewa.

Kwa mantiki hii, jamii yote na hasa watakaopeleka kesi au mashauri mahakamani ama wao binafsi au kupitia kwa mawakili wanatakiwa wawe na imani ya majaji wanaosikiliza kesi na wasiwe na shaka hata chembe kwamba haki itatendeka kutokana na umahiri wa majaji. Kukosekana kwa misingi hii ya kisheria na utawala bora, hofu na wingu la kutoaminiana litatanda, maamuzi ya majaji yatatiliwa mashaka na rundo la rufaa zitafumuka.

Kutokana na umuhimu mkubwa wa Majaji, utaratibu maalum wa kuteua majaji umeelezwa ndani ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 na tunanukuu Vifungu vifuatavyo vinavyoelezea kuhusu uteuzi wa Majaji ili kurahisisha ufahamu kwa wasomaji.

Kifungu 94 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinaeleza kwamba ''Jaji Mkuu atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahkama Kuu na baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahkama.''

Vile vile, Kifungu cha 94 (2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinaeleza kwamba ''Majaji wa Mahkama Kuu watateuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi ya Mahkama.''

Kifungu cha 94 (3) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 sifa za kuteuliwa kuwa Jaji au Kaimu Jaji wa Mahkama Kuu. Zifuatazo ni sifa za kuwa Jaji au Kamiu Jaji wa Mahkama Kuu Zanzibar:

**(a)** Awe na shahada ya Sheria ya Chuo Kikuu kinachotambuliwa au Chuo cha iana hiyo; na

**(b)** Awe amewahi kuwa Jaji wa Mahkama zilizofanana na hii kwa kesi zote za jinai na madai katika Tanzania au sehemu yeyote ya Jumuiya ya Madola ay Mahkama yenye mamlaka ya Rufaa kutoka Mahkama hizo; au

**(c)** Awe ni Mwanasheria wa Zanzibar au Tanzania kwa kipindi kisichopungua miaka saba; au

**(d)** Awe na uzoefu wa (a) na (b) kwa pamoja usiopungua miaka saba.

Kutokana na uwezo aliopewa na Katiba ya Zanzibar ya 1984, tarehe 29-11-2010, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Ali Mohamed Shein alifanya uteuzi wa majaji wa nne wa Mahkama Kuu. Wafuatao ni majaji walioteuliwa na Mheshimiwa Dk Shein:

1. Mhe: Abdul-hakim Ameir Issa
2. Mhe. Fatma Hamid Mahmoud
3. Mhe. Mkusa Isaac Sepetu, na
4. Mhe. Rabia Hussein Mohamed

Pamoja na Rais wa Zanzibar, Dk Shein kutekeleza masharti ya Katiba ya Zanzibar ya 1984, siku moja tu baada ya uteuzi wake, Chama cha Wanasheria Zanzibar kilimuandikia barua Rais wa Zanzibar, Dk Shein kumueleza kwamba hawakuridhika na utezi wa Majaji alioufanya na kumshauri kwamba asiwaapishe.



## Mawakili wampinga Dk Shein kuteua majaji

Salma Said, Zanzibar

CHAMA Cha Mawakili Zanzibar (ZLS) kimepinga uteuzi wa majaji wa Mahakama Kuu uliofanywa na Rais wa Zanzibar (SMZ), Dk Ali Mohammed Shein Novemba 29, mwaka huu wa 2010 na kuhoji uhalali wa uwepo wa Jaji Mkuu wa Zanzibar aliyestaafu.

Tayari ZLS kimemwandikia barua Dk Shein Novemba 30, ambayo Mwananchi ilifanikiwa kuiona nakala yake kikieleza kuwa hakijaridhishwa na uteuzi huo kwa kuwa haukuzingatia vigezo na kwamba, umekiuka sheria kwa kuwa hakijashirikishwa.

Barua hiyo ya ZLS ya Novemba 30, mwaka huu yenye kumbukumbu namba ZLS/IKULU/001 tayari imepelekewa Dk Shein ikiwa na saini ya Rais wa chama hicho, Yahya Khamis Hamad na mawakili 15 kwa niaba na wenzao zaidi ya 50, kupinga uteuzi huo wa majaji uliofanywa na Rais Dk Shein.

Novemba 29, mwaka huu Rais wa Zanzibar kwa mamlaka aliyopewa na katiba ya SMZ aliteua majaji wanne wa Mahakama Kuu pamoja na Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi, Haroub Sheikh Pandu.

Majaji wanne walioteuliwa ni Abdul-hakim Ameir Issa, Fatma Hamid Mahmoud, Mkusa Isaac Sepetu na Rabia Hussein Mohammed.

"Rais, katika uteuzi wako huo, ambao umetumia mamlaka uliyopewa na Katiba ya Zanzibar ya 1984 kifungu cha 94(2) na (3), Chama cha Mawakili hakina mashaka na uteuzi wa Abdul-hakim Ameir Issa, wala uteuzi wa Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi, Haroub Shehe Pandu. Mashaka yetu yapo katika uteuzi wa waheshimiwa kuanzia nambari 2 mpaka 4," Sehemu yabarua yao kwa Dk Shein ZLS inasomeka.

Hata hivyo, ZLS ilisema Rais hawezi kuwaelewa majaji wala hakuna sababu ya kumjua yeyote kati ya majaji wanne aliowateua, lakini wanachoamini uteuzi wake unatokana na ushauri aliopewa na Tume ya Utumishi ya Mahakama iliyoanzishwa chini ya Sheria Namba 13 ya mwaka 2003 ambayo Mwenyekiti wake ni Jaji Mkuu wa Zanzibar, Hamid Mahmoud Hamid pamoja na wasaidizi wa rais wengine katika sekta ya sheria.

"Rais, sisi mawakili ambao tumetia saini barua hii tukiwa ni wadau wakubwa katika sekta hii, tuna imani ▸4

**Mwananchi, Disemba 2, 2010**



8. Wekeza katika kuwalinda watoto wachanga na vijana dhidi ya VVU na magonjwa ya zinaa

Zanzibar Law Society

P.O.BOX 3186, Zanzibar, Tanzania. Bwawani Hotel – Ground Floor, Suite # 109. Tel/Fax +255 24 2234890 Mobile: +255 777 412669 Email: zls@zanlink.com

Tarehe: 30 Novemba 2010
Our Ref:ZLS/IKULU/001

**Kwa mujibu wa nakala ya Barua ya Chama cha Wanasheria, imeonekana wazi kwamba hawana mashaka na uteuzi wa Mheshimiwa Jaji Abdul-hakim Ameir Issa, lakini hofu kubwa ipo kwa washeshimiwa majaji watatu waliobakia.**

Vigezo vikubwa vilivyoelezwa na Chama cha Wanasheria Zanzibar na tunavinukuu kwamba ***''Nafasi ya Ujaji ni nafasi ya juu kabisa katika ngazi ya Mahkama zetu na pia ni nyeti. Utaalam uliobobea, rekodi iliyothibitika, umakini wa hali ya juu, kujiamini, uadilifu na umahiri wa hali ya juu - vyote kwa pamoja vinahitajika.''***


MOTO WATEKETEZA WATOTO WATATU WA FAMILIA MOJA
http://magazetismz.blogspot.com
Zanzibar Leo
KWA UKWELI NA UWAZI
GAZETI LA KILA SIKU BEI SH. 400/-
TOLEO NO.3256 JUMANNE, DISEMBA 21, 2010
Dk. Shein awaapisha Majaji

**Pamoja na malalamiko ya wanasheria Mheshimiwa Rais Dk Shein aliwaapisha majaji wote. Bila ya shaka Mheshimiwa Rais alitumia Kifungu cha 52 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinachoeleza kwamba**

***''Rais wa Zanzibar halazimiki kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeyote katika utekelezaji wa shughuli zake, isipokuwa kama sheria inaagiza vyenginevo.''***

**Hatuna mashaka hata kidogo ya Kifungu cha Katiba cha 52 kuhusu uwezo wa Rais wa kutofuata ushauri, lakini katika zama hizi za utawala bora ingelipendeza zaidi Mheshimiwa Rais akatafakari kwa kina malalamiko yaliyotolewa na Chama cha Wanasheria Zanzibar kuhusu uteuzi wa majaji.**

**Kufuatia kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar, nafasi ya chama cha upinzani ndani ya Baraza la Wawakilishi ya kuikosoa na kuielekeza Serikali haipo. Badala yake, Asasi za Kiraia kwa mfano Chama cha Wanasheria Zanzibar na Vyombo vya Habari ndio vinavyotegemewa kuikosoa na kuielekeza Serikali.**

**Kwa mtazamo wa maelezo tuliyoyatoa juu, inaonekana Utawala *(Executive)* haikuwatendea haki wananchi wa Zanzibar ukizingatia zaidi barua ya Chama cha Wanasheria Zanzibar kwamba uteuzi wa mmoja ya miongoni mwa majaji hawa ulifanywa bila ya kushauriwa na Tume ya Utumishi ya Mahkama kama Kifungu cha 94 (2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 ambacho tumekitaja hapo juu.**

**Suala kubwa linaloumiza vichwa wanasheria na jamii kwamba majaji hawa watakuwa huru *(independence)* katika maamuzi yao?**

# Kosa la kubaka

**UTANGULIZI:**

**Kosa la kubaka ni miongoni mwa makosa ya jinsia yaliyoorodheshwa katika Sheria ya Jinai ya Zanzibar No. 6 ya mwaka 2004.**

**Maana ya Kubaka *( Definition of Rape):***

**NI** tendo la mwanaume kumuingilia kimwili mwanamke au mtoto wa kike pasi na ridhaa yake. Mtu atachukuliwa kuwa amebaka pale ambapo atamuingilia mwanamke katika utupu wake wa mbele au wa nyuma pasi na mwanamke aliyeingiliwa kukubali kuingiliwa huko wakati tendo la kuingiliwa linafanyika. Hivyo itakua ni kosa kwa mwanaume kumuingilia mwanamke akifahamu kuwa mwanamke huyo hajaridhia kuingiliwa au atakapodharau au kutojali iwapo mwanamke huyo ameridhia au la. Ili kuthibitisha kuwa kosa la kubaka limetendeka vipengele vifuatavyo ni lazima vithibitishwe:-

- Kuingiza utupu wa mwanamme katika utupu wa mbele au nyuma wa mwanamke.
- Kukosekana kwa ridhaa ya mwanamke wakati tendo hilo linafanyika.
- Mwanamme kufanya tendo hilo akifahamu kuwa mwanamke anaemuingilia hajatoa ridhaa.

Kukosekana kwa Ridhaa ***(Absence of Consent):***

Tendo la kujamiiana litahesabiwa kuwa ni kubaka pale tu litakapokua limetendeka bila ya kuwepo kwa ridhaa ya mlalamikaji. Inaelezwa kuwa kiini cha kubaka ni kukosekana kwa ridhaa kutoka kwa mtu anaeingiliwa, na kwamba haijalishi waliofanya tendo hilo ni wageni, marafiki au wanandoa. Suala la msingi la kuzingatia ni juu ya mwanamke kuridhia kuingiliwa, aidha si lazima kuthibitisha kuwa mlalamikaji amechangia lakini inatosheleza kuthibitisha kuwa mlalamikaji hakuridhia kuingiwa na mlalamikiwa. Hivyo kuonesha kuwa mlalamikiwa alikua na nia ovu ya kutenda kosa hilo.

**Kosa la kubaka kisheria *(Offence of Rape under Penal Act):***

Kwa mujibu wa kifungu cha 125 cha sheria namba 6, 2004 Sheria za Zanzibar inaelezwa kuwa ni kosa kwa mwanaume kumuingilia mwanamke au mtoto wa kike, na kwamba mwanaume atachukuliwa kuwa amebaka iwapo atatenda mambo yafuatayo:-

- Iwapo mwanamke aliyemuingilia si mkewe, na iwapo ni mkewe basi wametengana kisheria na kwamba mwanamke huyo hakuridhia kuingiwa kwa wakati huo.
- Iwapo mwanamke huyo ameridhia lakini ridhaa hiyo imetokana na vitisho, nguvu na hata hofu ya kifo au kuumizwa kama yupo kizuizini.
- Iwapo ameridhia wakati ambapo hakua na akili timamu, au amelewa au ametumia madawa ya kulevya ambayo amepatiwa na mwanaume huyo au mtu mwengine.
- Iwapo ameridhia akifanywa aamini kuwa mtu anaYemuingilia ni mume wake wa ndoa ilhali mwaume huyo si mumewe
- Iwapo mwanamke ameridhia au hajaridhia na kwamba ana umri chini ya miaka 18, isipokuwa awe ni mume halali na kwamba hawajatengana kwa mujibu wa sheria.

Aidha mwanaume atachukuliwa kuwa ni mkosaji kwa kosa ka kubaka akiwa ni mtu mwenye wadhifa au mamlaka fulani, akatumia nafasi aliyonayo kumuingilia mwanamke au mtoto wa kike na akatumia mahusiano yaliyopo, au akamwekea vikwazo visivyo halali na akamuingilia mwanamke au mtoto wa kike.

Pia kama mwanaume atakua katika mamlaka au uangalizi wa watu walio kizuizini au sehemu nyengine ya uangalizi iliyowekwa kisheria au taasisi za wanawake na watoto, akatumia fursa kwa nafasi aliyonayo na akamuingilia mwanamke au mtoto wa kike, sheria inaendelea kueleza kuwa iwapo mtu atakua katika utawala au mfanyakazi wa hospitali, akatumia nafasi aliyonayo kumuingilia mwanamke au mtoto wa kike, na mwisho iwapo atakua ni kiongozi wa dini au mganga wa kienyeji akatumia nafasi aliyonayo kumuingilia mwanamke au mtoto wa kike kwa nia ya kutibu atakua ametenda kosa la ubakaji na kwamba sheria itamtia hatiani kwa kosa hilo.

**Ushahidi katika kuthibitisha kosa la kubaka:**

Inasisitizwa kuwa ili kosa la kubaka liweze kuthibitika kuingiza uume katika utupu wa mwanamke kunatosheleza na ushahidi wa kujihami kama majeraha ya mwili hayana umuhimu kuonesha kua kosa la kubaka lilitendeka. Hailazimiki kuingiza sehemu yote ya utupu wa mwanamme katika utupu wa mwanamke ili kuonesha kua kuingilia kumefanyika au hata kuacha mbegu za kiume, sehemu ndogo inatosheleza kuonesha kuwa tendo hilo limefanyika kama inavyoelezwa katika kesi ya Hughes (1841) 9 C&P 752

*"It is necessary to prove sexual intercourse whether natural or unnatural, it shall not be necessary to prove the completion of the intercourse by the emission of the seed, but the intercourse shall be deemed complete upon proof of penetration only."*

**Kubaka kwa kundi *(Gang Rape):***

Sheria imezingatia tendo la kubaka linaofanywa kwa kushirikiana, pale ambapo itathibitika kuwa kosa limefanywa na mtu mmoja au zaidi basi kila mhusika ama awe ametenda binafsi au amesaidia kutendeka kwa kosa la kubaka atachukuliwa kuwa amehusika kubaka na mtu atakaetiwa hatiani kwa kosa la kubaka kwa kundi atapewa adhabu ya kifungo cha maisha gerezani bila ya kujali mchango gani aliutoa katika kutenda kosa hilo na haijalishi kama mtu huyo atakua ni mwanamke au mwanaume kama ambavyo Kifungu cha 127 (1) kinavyoelekeza.

**Kujaribu kubaka *(Attempted Rape):***

Kwa mujibu wa Kifungu cha 128 cha Sheria namba 6,2004 mtu ambae atajaribu kubaka atakua ametenda kosa hilo na kwamba adhabu yake itakuwa ni kifungo cha maisha, iwapo atamtishia mwanamke au mtoto wa kike kwa nia ya kumuingilia, au mtu aliye na mamlaka akatumia mamlaka yake kumshawishi mtoto wa kike au mwanamke na kumshawishi kwa lengo la kumuingilia kimwili. Hata hivyo mtu hatatumikia kifungo cha maisha iwapo katika kujaribu kwake kubaka atadanganya kwa mwanamke au mtoto wa kike kwa nia ya kupata ridhaa yake na iwapo atajifananisha na mume halali wa mwanamke au mtoto wa kike, kwa kutoa ridhaa akiamini kuwa mtu huyo ni mumewe, na kwamba adhabu itolewayo katika mazingira hayo ni Kifungo kisichopungua miaka ishirini.





10. Wekeza kwa watoto wenye ulemavu

### Adhabu kwa kosa la kubaka( *Punishment for Rape)*

Kifungu cha 126 (1) kinatoa ufafanuzi juu ya adhabu itolewayo kwa kosa la kubaka, na pale itakapothibitika kua mtu ametenda kosa hilo basi atapewa adhabu ya kifungo cha maisha gerezani na iwapo ikiwa kwa namna yoyote ni kifungo basi kiwe ni kifungo kisichozidi miaka thelathini gerezani na malipo na pia kwa amri ya ziada ya mahkama atalazimika kulipa fidia kwa muathirika au mtu aliyebakwa kutokana na majeraha aliyoyapata au athari za kisaikolojia ambazo mtu huyo amepata. Hata hivyo kifungu kidogo cha 2 kinaeleza kuwa adhabu hiyo haitatolewa iwapo kosa hilo litafanywa na mtoto wa kiume akiwa mwenye umri wa miaka kumi na nane au chini yake na iwapo ni:-

- Mkosa wa kosa la kwanza, atahukumiwa kifungo cha mwaka mmoja katika mahkama ya watoto au kufanya kazi za kutumikia jamii.
- Ikiwa ni mkosa wa kosa la pili, atahukumiwa kifungo cha muda wa miezi kumi na mbili.
- Ikiwa ni mkosa wa kosa la tatu na ni mhalifu mzoefu atahukumiwa kifungo cha maisha kwa mujibu wa Kifungu cha kwanza.

### Kosa la Kubaka kimataifa:

Mkataba wa kimataifa wa ICC *(Rome Statute)* umetambua kosa la kubaka kuwa ni miongoni mwa makosa dhidi ya ubinaadamu *(crimes against humanity)* yanayopelekea kuzuia utu na heshima ya binaadamu ikiwemo udhalilishaji wa maisha ya binaadamu kama ambavyo inaainishwa na ibara ya saba ya mkataba huo. Inaelezwa kwamba msingi wa kutambua kosa la kubaka kimataifa umetokana na kesi ya *Prosecutor v. Akayesu,* ambapo mahkama ya kimataifa ya Rwanda ilimuona mtuhumiwa Paul Akayesu ana hatia kwa makosa dhidi ya ubinaadamu ikiwemo kubaka, chini ya sheria ya Mahkama ya Kimataifa ya Rwanda *(ICTR Statute)* ambayo imeainisha ubakaji kuwa ni sehemu ya mfululizo wa matukio ya mashambulizi dhidi ya raia na kutoa athari kuwa ubakaji unazingatiwa kama makosa mengine dhidi ya ubinaadamu na kutoa msingi kua ubakaji unapelekea mauaji ya kimbari (*genocide*) kwa mujibu wa sheria za kimataifa.

Vilevile kesi hii imetoa ufafanuzi mzuri kuhusiana na matumizi ya silaha na zana mbali mbali zitumikazo kuwadhalilisha wanawake kimapenzi, na kwa msingi huo mahkama imeweka wazi kuwa mtu atakua ametenda kosa la kubaka hata kwa kutumia zana nyengine kuingiza katika utupu wa mwanamke na haitalazimika kuingiza uume wa mwanamme katika utupu wa mwanamke ili kuthibitisha kosa la ubakaji katika sheria za kimataifa

Kwa mujibu wa Ibara ya 7 (g) ya Mkataba wa ICC, 1998 kosa la kubaka limeingizwa ikiwa ni miongoni mwa makosa dhidi ya ubinaadamu, ikimaanisha iwapo ubakaji utafanywa kama ni sehemu ya mfululizo wa mashambulizi ya kupangwa dhidi ya umma na kwa kufahamu lengo la mashambulizi hayo. Aidha mkataba wa ICC ni muhimu kwavile umetanua maeneo muhimu yanayohusisha makosa dhidi ya wanawake zaidi ya ubakaji. Pia umeweka wazi kwamba makosa kama vile udhalilishaji wa kimapenzi, umalaya wa kulazimishwa, mimba za lazima na mengineyo yataadhibiwa chini ya sheria ya kimataifa.



**Mashine ya DNA**

### Viini (*Elements*) vinavyojenga kosa la Kubaka chini ya Mkataba wa ICC:

Mkataba wa ICC kupitia maamuzi ya Mahkama za ICTY na ICTR imeweza kutoa tafsiri muafaka ya kosa la kubaka ambayo imeingiza mambo yafuatayo:-

- Iwapo mhalifu atamuingilia mtu mwengine katika sehemu yoyote ya mwili wake hata kwa kuingiza sehemu ndogo ya sehemu yake ya siri katika mwili wa mlalamikaji au kwa kuingiza katika sehemu ya siri ya mbele au nyuma ya mlalamikaji kwa kutumia zana au sehemu yake yoyote ya mwili.
- Uvamizi utafanywa kwa kutumia nguvu, vitisho na hata kulazimisha, kama vile hofu ya kuwepo fujo, kizuizi, kudhalilishwa kisaikolojia, au kutumia madaraka vibaya
- -Uvamizi utafanywa kwa kutumia nguvu, vitisho na hata kulazimisha, kama vile hofu ya kuwepo fujo, kizuizi, kudhalilishwa kisaikolojia, au kutumia madaraka vibaya dhidi ya mlalamikaji au mtu mwengine au kwa kutumia mazingira ya fujo au uvamizi kutenda kosa hilo dhidi ya mtu ambae hawezi kutoa ridhaa inayokubalika.

Hivyo Vipengele muhimu vilivyoainishwa ni kuwepo kwa mazingira ya kutumia nguvu na mtu kutoweza kutoa ridhaa kwa tendo la kuingiliwa.

### Hitimisho:

Kosa la kubaka ni miongoni mwa makosa makubwa yanayokwenda kinyume na heshima na utu wa mwanadamu hususan mwanamke. Makosa ya aina hii yanapofanyika huacha athari mbalimbali zikiwemo za kimwili na kisaikolojia. Kwa kawaida athari itokanayo na kubakwa huacha maumivu yenye kuendelea kwa muathirika. Hivyo washtakiwa wa makosa ya aina hii wanastahiki adhabu kubwa na kwamba ni juu ya waathirika wenyewe pamoja na jamii kutoa mashirikiano kutoa ushahidi na kuhakikisha kuwa wahusika wanatiwa hatiani na kupata adhabu zinazostahiki.

# Kituo kimeadhamisha Siku ya Kuzaliwa Prof. Haroub Othman

MNAMO tarehe 4 Disemba, 2010 Kituo cha Huduma za Sheria cha Zanzibar kiliadhamisha siku ya kuzaliwa kwa mmoja wa waasisi wake Profesa Haroub Miraji Othman. Kama ilivyojengeka katika shughuli zake, siku hiyo huwa ni siku ya kusherehekea maisha yake na mchango wake kwa jamii ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Sherehe hiyo iliyofanyika katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa za Zanzibar (SUZA) ilifunguliwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Iddi na mada nzuri kutolewa na Profesa Issa Shivji; Mhe. Fatma Fereji na Mhe. Mahadhi Juma Maalim. Katika sherehe hizo mada kuu iliyojadiliwa ilikuwa ni kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar.

Pamoja na mada hii, vile vile kulikuwa na salamu kutoka sehemu mbali mbali ndani na nje ya nchi ikiwa zote zinahusu maisha na mchango wa Profesa Haroub Othman. Moja ya salamu hizo ni zile zilizopokelewa kutoka Cologne, Ujerumani. Salamu hizi zilitoka kwa mdogo wake Bw. Othman Miraji Othman, ambaye ni mtangazaji maarufu wa Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Ujerumani Deutsche Welle. Kwa sababu ya uzito wa salamu hizo na maudhui yake, Jarida letu linazitoa kama zilivyokuja:

**Salamu za Bw. Othman Miraji Othman**
**Cologne, Ujerumani**
**(4 Desemba, 2010)**




*Bw. Othman Miraji Othman (Katikati) akiwa na Marehemu Prof. Haroub Othman (Kulia) na Prof. Chris Maina Peter (kushoto) katika Hoteli ya Bwawani, Unguja kuhudhuria Semina iliyotayarishwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar.*

**Ndugu Nyote Waheshimiwa,**

**Mwenyezi** Mungu angemrefushia maisha hapa duniani, leo Profesa Haroub Miraji Othman angekuwa na umri wa miaka 68 na siku nne hivi; na leo ni mwaka mmoja na zaidi kidogo ya miezi mitano tangu atutoke hapa duniani. Licha ya huzuni kubwa ilioikumba familia yake- mkewe, Profesa Saida, mtoto, wajukuu, mjomba , ndugu zake, jamaa zake na marafiki zake, hata hivyo, wote wanafarijika kwamba yale yanayozungumzwa ukumbini hapa leo pamoja na yale yaliyojiri katika Visiwa vyetu vya Zanzibar tangu alipofariki Profesa ni mambo aliyoyatamani marehemu yatokee na kuomba ayashuhudie kwa macho yake, hata ikiwa mwishoni wa maisha yake. Lakini Mwenyezi Mungu hajajaalia iwe hivyo. Mola ndiye mjuzi wa yote.

Si muda mfupi kabla hajafariki, marehemu alishiriki katika mkusanyiko wa Wazanzibari wakati wa kuzinduliwa kitabu kilichozungumzia juu ya maisha ya Maalim Seif Shariff Hamad, ambaye sasa ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, na Sheikh Ali Sultan Issa. Ni Profesa aliyepewa jukumu la kutoa mapitio juu ya kitabu hicho kiitwacho *Race, Revolution and the Struggle for Human Rights in Zanzibar:* Memoirs of Ali Sultan Issa and Seif Sharif Hamad, kilichohaririwa na Profesa Thomas G. Burgess na kuchapishwa na Ohio University Press ya huko Athens, Ohio Marekani mwaka 2009. Wasimulizi hao wawili wa kitabu walichangia sana katika historia ya kisiasa ya Visiwa vya Zanzibar. Si ajabu kwamba mkusanyiko huo wa watu walio na mikondo mbali mbali ya kisiasa ulikuwa wa kuvutia na yaliyozungumzwa yalikwenda mbali zaidi na maisha ya wahusika hao wawili. Watu wengi walioondoka baada ya kongamano hilo walipata hisia kwamba sasa Zanzibar ilikuwa ikielekea katika mabadiliko, na kwamba huenda yakawa ni mabadiliko ya kheri kwa Wazanzibari wote.

Saa 16 baada ya kongamano hilo Profesa Othman aliaga dunia, bila maumivu, ubavuni mwake mkewe, tena akiwa katika nchi yake aliyoipenda - Zanzibar. Tunawashukuru wale wote waliofuatana na Haroub kwa wema katika maisha yake.

Tangu mkusanyiko ule, na kila siku zikienda, Visiwa

**Inaendelea Uk. 13**

# Kituo kimeadhimisha Siku ya Kuzaliwa Prof. Haroub Othman

**Inatoka Uk. 12**

vyetu vinaelekea katika nuru alioitamani Haroub izagae, nuru itakayowaongoza Wazanzibari wote kutumia nguvu zao zote- za hali, mali na akili - kujenga mustakbali mpya wa nchi yao na vizazi vya baadae, badala ya kutumia nguvu hizo katika misuguano na malumbano ya kisiasa yasiokwisha. Wazanzibari wamepoteza wakati mwingi katika mambo hayo, na sasa wamegundua kwamba bila ya kuwa na Umoja, hasara ni kwa wao wote, na watu wa nchi nyingine wanawacheka na kuwadharau. Kura ya Maoni ya wananchi ilitoa ridhaa kubwa ya kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa,, yote yamedhihirisha kupea kisiasa kwa Wazanzibari na pia kuhakikisha kwamba wanataka kusonga mbele na kuangalia mustakbali kwa ujasiri, wakiwa na imani kwamba Umoja wao na udugu wao uliojengeka kwa makarne kwa makarne kutokana na kuzaliana kwa familia zao na koo zao mbali mbali hautatetereka tena. Wameonesha kwamba wanaweza kutafautiana kisiasa, lakini hawatakubali kamwe kuonesheana visu, nondo, magongo, seuze mitutu ya bunduki.

Angekuwepo hapa leo, Profesa angewapongeza wale wote waliochangia katika kuchomoza jua hili, jua linalotoa matumaini mazuri kwetu sote. Mwenyezi Mungu ajaalie viongozi wetu katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa wawe na nguvu na hekima kuweza kuyafikia hayo malengo waliyoyawekea kwa nchi yetu, tena kwa upesi kama iwezekanavyo.

Haroub alikuwa msomi, lakini usomi wake hajataka umalizikie vitabuni, madarasani katika vyuo vikuu na kwenye makomgomano. La hasha! Alikuwa na "*Vision*", upeo wa fikra juu ya wapi anataka watu wafike, na hasa kuwasaidia watu wajikomboe na unyonge wao na dhuluma zinazowakabili. Hali hiyo ndio iliomchochea kuwa mmoja wa waasisi wa Kituo cha Huduma za Sheria Visiwani Zanzibar na Pemba. Aliyapima mafanikio yake na yale ya kufikia malengo ya Kituo hicho. Na kile kilichomchochea zaidi ni kupinga ile dhuluma ya kuwaona Wazanzibari wanahasimiana kisiasa kwa kiwango cha kutaka hata kuangamizana! Ameondoka, lakini, ameiwacha Taasisi hii katika hali thabiti, ikiwa katika mikono ya wanasheria vijana, makini na wenye ghera ya kuwatumikia watu, kama alivokuwa yeye mwenyewe, wakakamavu katika kutetea haki za kila Mzanzibari, na kwamba Sheria ndio iwe Bwana wa kila kitu.

Profesa, licha ya kuhitimu sheria, alipenda siasa. Nyumbani kwa wazee, mazungumzo yalikuwa siasa kila wakati. Na licha ya kuwa kila mmoja wetu ndani ya familia alikuwa na mtizamo wake huru, kulikuweko uvumilivu mkubwa, kila mmoja akiwa huru kujiunga au kukipendelea chama chochote cha siasa. Serikali ya Umoja wa Kitaifa sio ngeni katika familia yake, ilianzishwa na wazee wetu ndani ya familia tangu mwaka 1957, katika uchaguzi wa kwanza Visiwani.

Nini ambacho Haroub angefurahi kukiona baada ya kuundwa Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa hapa Zanzibar? Tunaamini angeitakia kila la kheri, angependelea iimarishe umoja na makongamano ya kitaifa yaliochomoza, angetaka serikali mpya ijikite katika kutanzua tatizo la umasikini nchini, kuuimarisha uchumi, kutilia nguvu suala la elimu ilio bora kwa watoto wetu na kuwapunguzia wananchi urasimu mwingi. Angetaka serikali mpya iwe ya watu wote, na kila mwananchi awe na fahari na Serekali hiyo, na pia iwe mlinzi wa kila mwananchi anayekoseshwa haki yake kwa makusudi au vinginevyo. Licha ya hayo, angetaka Zanzibar iwe na Katiba mpya ya kisasa, ilioridhiwa na watu wake, na pia kuanzishwe mchakato wa kutafuta mfumo wa Muungano wa Tanzania utakaowaridhisha watu wengi wa kila upande wa Muungano. Haifichiki kwamba Profesa alikuwa mtetezi wa Muungano si wa Tanzania tu, lakini wa Afrika nzima, lakini wa mfumo utakaokubaliwa na watu wengi wa kila upande.

Kwa kumalizia, Zanzibar tunayoipenda, tuilinganishe na kitongoji cha zamani cha Ebrahim Hussein katika Ngao Yake ya Jadi. Yeye hajaisemea Zanzibar wakati huo alipoandika, bila ya shaka, lakini maneno yake tunaweza kusema yanasikika hivi sasa, huenda angalau yanafikia hadi Mnara wa Chumbe. Mtanzania huyo aliandika hivi:

"Kitongoji hiki kilikuwa kinaitwa Kitongoji-Masononi, kilikuwa na watoto, watoto wazuri, na wenye wingi shani. Na kila aliyewaona watoto Masononi, Moyo wake uliingiwa gharba, mapenzi na imani.

Miaka ikapita, miaka ikapita, miaka ikapita; Watu wakaoana, watu wakazaana, na mali ikazidi. Lakini moyoni simanzi ikatamba, simanzi haini kwa kila mwana-Masononi.

Hatua si hatua, ni mdomo na pua. Liliishi Kitongoni joka la vichwa sabini; Na kila aliyeliona joka hilo maluhuni, moyo wake 'liingiwa hofu na mashaka ya kiinsani.

Miaka ikapita, miaka ikapita, miaka ikapita; Simanzi ikatambazika, Huzuni ikatandazika, na majonzi yakazidi, kwani ilikuwa tabia makini, kila mwaka ukibaini, Joka hushuka kijijini, kuchukuwa mali na binti mzuri mmoja.

Huyu nyoka n'ambieni ni joka kubwa la zamani, linavyo vichwa sabini, na kila shingo yake lina lake Koya „Ama yafaa sasa tumtafuteni ..."

Joka lilokuwa Kisiwani kwetu nimgawanyiko wetu. Tumelitafuta, tumeligundua Joka hilo, lilobaki sasa ni kuliangamiza lisirejee tena katika Zanzibar yetu.

Iishi Zanzibar, Iishi Tanzania, na Mwenyezi Mungu awarehemu wote waliotangulia mbele ya haki na waliopigania siku kama ya leo ichomoze ... Ameen.

# ZEC yatakiwa kuendesha uchaguzi kwa uwazi



*Wafuasi wa vyama vya siasa wamekusanyika nje ya Hoteli ya Bwawani wakisikiliza matokeo ya uchaguzi*

**TUME** ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imetakiwa kufanya kazi kwa uwazi zaidi ili kujenga imani ya wapiga kura kuamini matokeo bila ya kuwa na chembe ya shaka.

Ushauri huu umetolewa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) katika ripoti ya uangalizi wa zoezi la uchaguzi wa Zanzibar uliofanyika Oktoba 31, 2010.

Ripoti ilisema kwamba pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na ZEC lakini tatizo kubwa lililojitokeza ni kukosekana kwa uwazi kwenye majumuisho ya kura katika ngazi ya Wilaya na Taifa.

''Mawakala wa vyama vya siasa na waangalizi wa zoezi la uchaguzi wa ndani na nje ya nchi walinyimwa nafasi ya kushiriki katika majumuisho ya kura za rais wa Zanzibar,'' ilisema ripoti ya ZLSC.

Ripoti ilisema kwamba kitendo cha kutoruhusiwa wawakilishi au waangalizi kushuhudia zoezi la majumuisho lileta shaka na kusababisha mtafaruku wa baadhi ya wafuasi wa cha Chama cha Wananchi (CUF) kuvamia katika kituo cha utangazaji wa matokeo kiliopo katika hoteli ya Bwawani.

Vile vile, ripoti ilisema kwamba ZEC ijitahidi kuboresha uandikishwaji wa wapiga kura na kuondoa vikwazo vilivyowanyima nafasi baadhi wa wapiga kura kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutokuwa na vitambulisho vya ukaazi vya mzanzibari (*ZAN-ID*).

Inadaiwa kiasi cha watu laki moja (100,000) waliostahiki kupiga kura hawakuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Ripoti ilisema tathmini ya uchaguzi ya ujumla ilionyesha kwamba uchaguzi wa Zanzibar kinyume na chaguzi za nyuma ulikuwa wa amani na utulivu.

Ilisema kwamba wananchi walipata fursa ya kuchagua viongozi wanaowataka na kwamba kulikuwa na uwazi wa hali ya juu sana katika ngazi zote isipokuwa kwenye majumuisho ya kura za rais wa Zanzibar katika ngazi ya Taifa.

Taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi ziliipongeza ZEC katika zoezi la uendeshaji wa upigaji kura.

Lakini ripoti hizo zilionyesha kasoro kubwa ya kutokuwa na uwazi katika majumuisho ya kura za rais wa Zanzibar na kuishauri Tume kuwaruhusu wawakilishi wa wagombea na waangalizi kushuhudia majumuisho ili kuondoa shaka.

Katika uchaguzi wa nne wa vyama vingi, mgombea wa urais wa Zanzibar kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Dk Ali Mohamed Shein alichaguliwa kuwa rais wa Zanzibar.

Chaguzi za vyama vingi zilizofanyika Zanzibar tokea baada ya Mapinduzi ya 1964 ni uchaguzi wa mwaka 1995, 2000 na 2005.

Katika chaguzi zilizopita, Zanzibar ilishuhudia vurugu na kusababisha umwagaji wa damu na baadhi ya vyama na wagombea kutoyatambua matokeo ya uchaguzi kwa madai kwamba yalichakachuliwa na ZEC.

# Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (1999)

**Huu ni mfululizo wa makala za Haki za Watoto zinazochapishwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar kwa kushirikiana na *Save the Children***

**Kipengele cha 1**
Mkataba huu ni wa nchi wanachama wa Muungano wa Afrika. Mkataba huu hautazuia vipengele vyovyote katika sheria za nchi wanachama au mikataba ya kimataifa vinavyotekeleza vizuri zaidi haki na ustawi wa mtoto.

Mkataba huu unahamasisha kuachwa kwa mila, desturi na imani za kidini zinazopingana nao.

**Kipengele cha 2**
Kila mtu mwenye umri wa miaka chini ya 18 ana haki zote zinazotajwa na mkataba huu.

**Kipengele cha 3**
Una haki ya kulindwa dhidi ya kubaguliwa. Hii inamaanisha kuwa hakuna mtu yeyote anayeweza kukutendea vibaya kwa sababu ya rangi, jinsia, dini, kuongea lugha tofauti, ulemavu, utajiri, umasikini n.k

**Kipengele cha 4**
Watu wazima wote wanatakiwa kukutendea vizuri.

Kama unaweza, una haki ya kupewa nafasi ya kutoa maoni yako kuhusiana na mambo yeyote ya kiserikali na ya kimahakama yanayokuhusu.

**Kipengele cha 5**
Una haki ya kuishi na kutohukumiwa adhabu ya kifo ukipatikana na hatia ya kuvunja sheria za nchi.

**Kipengele cha 6**
Una haki ya kuwa na jina, kuandikishwa baada tu ya kuzaliwa na uraia wa taifa lako.

**Kipengele cha 7**
Una haki ya kutoa maoni, kusikilizwa na maoni yako kufanyiwa kazi, ili mradi tu huvunji haki za wengine.

**Kipengele cha 8**
Una haki ya kuwa pamoja na rafiki zako, kujiunga nao au kuanzisha kikundi cha watoto, ili mradi tu huvunji sheria.

**Kipengele cha 9**
Una haki ya kufikiria utakacho na kuchagua dini uipendayo, kwa kufuata ushauri wa wazazi wako.

**Kipengele cha 10**
Una haki ya kuwa na mambo yako ya binafsi mfano kutotafutiwa marafiki na kuheshimiwa utu

wako. Unaweza pia kuitetea haki hii kwenye vyombo vya sheria.

Wazazi au walezi wako pia wana haki ya kusimamia tabia yako.

**Kipengele cha 11**
Una haki ya kupata elimu.

Elimu hii inatakiwa ;

- **a.** kukujenga utu na uwezo wako kadri inavyowezekana.
- **b.** kukuhamasisha kuheshimu haki za binadamu zinazotajwa na mikataba mingine ya Afrika na ya kimataifa.
- **c.** kulinda na kuendeleza mila, desturi na tamaduni nzuri za kiafrika.
- **d.** kukuandaa kwa maisha ya kuwajibika katika jamii ya watu huru, kuvumilia watu na mawazo tofauti na yako na kuwaheshimu watu wote.
- **e.** kulinda utaifa na mipaka ya mataifa mbali mbali.

Serikali inatakiwa ;

- **i.** kukupa elimu ya msingi bure.
- **j.** kuhamasisha maendeleo ya elimu ya sekondari na taratibu kuifanya kuwa ya bure kwa watoto wote.
- **k.** kuifanya elimu ya juu bure na inayoweza kufikiwa na kila mtu kulingana uwezo wake.
- **l.** kuhamasisha mahudhurio mazuri shuleni na kupunguza kwa idadi ya watoro.
- **m.** kuchukua hatua maalum kuhakikisha wasichana, watoto wenye vipaji na wale wanaohitaji msaada wanapata elimu.

Wazazi au walezi wako wana haki ya kukuongoza katika kupata haki hii ya elimu.

Unapokuwa unaadhibiwa, iwe nyumbani au shuleni, haitakiwi kukudhalilisha au kukuvunjia utu wako. Iwapo utapata ujauzito ukiwa bado ni mwanafunzi, una haki ya kuendelea na masomo kulingana na uwezo wako.

**Kipengele cha 12**
Kulingana na umri wako, una haki ya kucheza na kupumzika.

**Kipengele cha 13**
Kama wewe una ulemavu, uwe wa kiakili au kimwili, una haki ya uangalizi maalum, michezo na elimu ya kukusaidia kujiendeleza na kuishi maisha kamilifu.

**Kipengele cha 14**
Una haki ya kuwa na afya bora ya kimwili, kiakili na kiroho kadri inavyowezekana,

Serikali inatakiwa kuchukua hatua;

- **a.** kupunguza magonjwa na vifo kwa watoto.
- **b.** kukupa huduma za afya ya msingi, mfano chanjo na kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukizwa kama vile kipindu pindu.
- **c.** kuhakikisha unapata chakula cha kutosha na maji salama ya kunywa.

***Inaendelea toleo lijalo.......***

Save the Children®
**P.O.Box 1267, 2nd Floor, Tiger House**
**Majestic Cinema/Vuga Street.**
**Zanzibar, Tanzania**
***www.savethechildren.org.uk***

Jarida la Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

# SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi

Ifanye haki
Iwe shauku

Toleo Na. 004 Jarida la kila miezi mitatu Oktoba - Disemba, 2010

# Akatwa sikio na mashoga zake



Maryam Ali akatwa sikio

**MARYAM** Ali Abdallah (16) mkaazi wa Mkwajuni, Wilaya ya Kaskazini ''A'' Mkoa wa Kaskazini Unguja, amekatwa sikio la mkono wa kulia na mashoga zake wawili kwa kutumia kiwembe na amelipwa fidia ya shilingi hamsini elfu (50,000/).

Hakimu wa Mahkama ya Wilaya ya Mkokotoni, Mheshimiwa Yahya Ussi Yahya, aliamuru waliotenda kosa hilo Fatma Jamal Salim na Acha Kheri Mtwana wenye umri wa miaka kumi na nane walipe fidia ya shilingi hamsini elfu kufuatia kukiri kosa la kumkamata Maryam na kumkata sikio kwa kutumia kiwembe ndani ya nyumba yao.

Washtakiwa hao kwa pamoja walimkamata Maryam na kumkata sikio kwa sababu alihama kutoka maskani yao na kuhamia maskani nyengine na kumtuhumu kwamba alikuwa anapeleka ''chokochoko'' za ugomvi baina ya vikundi viwili hivyo.

Hakimu Yahya aliwaamuru washtakiwa kulipa faini ya shilingi hamsini elfu (kila mmoja kulipa shilingi 25,000/-) au kutumikia kifungo cha miezi sita Chuo cha Mafunzo. Washtakiwa walilipa faini.

Tukio liliripotiwa Kituo cha Polisi Mkokotoni kabla ya kesi kusikilizwa mahkamani na kutolewa uamuzi siku hiyo hiyo baada ya washtakiwa kukiri kosa.

Ripoti ya awali ya uchunguzi wa kitaalamu ilionyesha kwamba kipande cha sikio kilichokatwa hakitoweza kuunga kwa sababu kimepoteza hisia (*autolysis*).

Maryam hakuridhika na adhabu iliyotolewa na amesema atakata rufaa kupinga adhabu ambayo walisema ni ndogo mno.

# Mwanamke aliyepotea kwa muda mrefu aonekana

**MWANAMKE** aliyepotea kwa muda mrefu na kudhaniwa amefariki, Bi Lawama Abdalla, ameonekana hivi karibuni na kusababisha jamaa zake kutokwa na machozi ya furaha.

Taarifa kutoka kwa jamaa zake zilisema kwamba ndugu yao alipokuwa na umri wa miaka (14) alipewa uzito na mwanajeshi na baadaye kuolewa.

Baadaye walisafiri kwenda Tanzania Bara na katika mazingira ya kutatanisha ilidaiwa kwamba mwanamke huyo alichukuliwa na mumewe kutoka nyumbani kwao wakati wa usiku mkubwa na kwenda pahali pasipojulikana.

Mwanamme alipoulizwa alisema hatambui taarifa zozote. Lakini watoto wa mwanamke walimuona mama yao akichukuliwa na mwanajeshi huyo lakini hawakujua wapi walikwenda na kwa madhumuni gani.

Taarifa zimeelezwa kwamba jeshi huyo alikamatwa na kufikishwa Mahkamani kwa tuhuma za kuua lakini ushahidi haukutosheleza na aliachiwa huru.

Imeelezwa kwamba mwanamke huyo alitupwa katika msitu mkubwa na akaokotwa na bibi mmoja mwenye zaidi ya miaka sabini na kuishi naye kwa kipindi kirefu kabla ya kuweza kupata msaada wa kurudi Zanzibar na kuungana na jamaa zake.

Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kwa kushirikiana na polisi walifuatilia suala hilo na kufanya mawasiliano baina ya mwanamke huyo na jamaa zake Zanzibar. Hatimaye, aliweza kurudi Zanzibar.

# Adai kunyimwa dhamana kwasababu mbara

**OTHUMANI** Kilenzi Magina anayetuhumiwa kwa kosa la mauaji amedai amenyimwa dhamana kwa kigezo kuwa asili yake ni kutoka Tanzania Bara.

Katika barua yake aliyompelekea Jaji Mkuu Zanzibar na nakala kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Katibu Mkuu wa Wizara ya Sheria na Katiba na Mkurugenzi wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar alisema ana haki za msingi.

''Nina haki za msingi ikiwemo kusikilizwa kesi kwa haraka, afya yangu ni mbaya na nateseka kwa jambo ambalo sijalifanya,'' ilisema barua hiyo iliopitishwa kwa Kamanda Mkuu wa Chuo cha Mafunzo Kilimani (Kiinua miguu).

Alidai kwamba upelelezi wa kesi umekamilika lakini hakuna hata shahidi aliyejitokeza kutoa ushahidi dhidi yake. Alisema anadaiwa kutenda kosa la mauaji Juni 6, 2007.

Alisema kwamba ucheleweshaji wa kesi ni kwenda kinyume na utawala wa sheria na haki za binadamu.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 150 (1) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Namb. 7/2004 mtu anaweza kupewa dhamana isipokuwa wanaoshtakiwa kwa makosa ya mauaji, uhaini, wizi wa kutumia nguvu au kupatikana na silaha kinyume na sheria au usafirishaji wa madawa ya kulevya.

Mahkama ina uwezo wa kutoa dhamana inapofika miezi tisa kwa kosa la mauaji ikiwa upelelezi haujakamilika.